



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA  
OFISI YA RAIS



TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA

HALMASHAURI YA MJI TUNDUMA

TANGAZO LA NAFASI ZA KAZI YA UFUNDI  
20/12/2022

Halmashauri ya Mji Tunduma imetenga fedha kwa ajili ya kugharamia ujenzi wa jengo la **Mkurabit** kwa mwaka wa fedha 2022/2023. Halmashauri inakusudia kutumia fedha hizo kugharamia ujenzi wa jengo hilo kwa utaratibu wa force account, ili kufanya kazi hiyo Halmashauri inatangaza nafasi za mafundi wenye sifa kwa kuzingatia masharti yafuatayo:-

1. Mwombaji awe Mtanzania mwenye makazi yanayoleweka, atatakiwa kupitisha Maombi yake kwa Mtendaji wa kata anakoishi.
2. Mwombaji atatakiwa kuwa na uzoefu wa kazi za ujenzi wa majengo ya serikali, kuthibitisha hili muombaji atatakiwa kuorodhesha miradi aliokwisha tekeleza ikiambatana na mahali ilipo, jina na namba za simu za wamiliki wa miradi hiyo.
3. Mwombaji anatakiwa kuwa na kiwango cha chini kabisa cha elimu ya darasa la saba na ujuzi wa kazi za ufundi wa majengo ya serikali, uwezo wa kusoma ramani za majengo ni sifa ya msingi.
4. Mwombaji atatakiwa kuthibitisha kuwa anazo nyenzo muhimu kufanya kazi, kuthibitisha hili atatakiwa kuorodhesha nyenzo za kufanya kazi alizonazo.
5. Kazi hii ni kubwa inahitaji mafundi wa kutosha ili ikamilike ndani ya muda, hivyo mwombaji anatakiwa kuainisha idadi ya mafundi atakaoweza kuwapata na kuwatumia katika kutekeleza mradi ya ujenzi.
6. Mwombaji anatakiwa kuanisha katika Maombi yake gharama za ufundi wa jengo kwa kuitia ramani na michanganuo ya mahitaji ya ufundi atakayopewa.
7. Waombaji wanashauriwa kukagua eneo la ujenzi na michoro kabla ya kukokotoa gharama za ujenzi.
8. Kwa maelezo zaidi waombaji wanaweza kununua na kusoma nyaraka za zabuni katika ofisi ya Manunuzi na ugavi kwa malipo ya shilingi 30,000/= kwa kila ombi, Fedha ambazo hazitarudishwa hata kama mwombaji hata shinda zabuni.
9. Ofisi hailazimiki kukubali bei za ufundi zenye gharama ya juu au chini .

10. Maombi yote yaandikwe kwa lugha ya Kiswahili na kufungwa katika bahasha na kutumwa kwa:-

**MKURUGENZI WA MJI  
HALMASHAURI YA MJI TUNDUMA  
S.L.P 73,  
TUNDUMA.**

11. Mwisho wakupokea maombi ni tarehe **27.12.2022**, saa **04:00** asubuhi na Maombi yote yatafunguliwa hadharani siku na muda huo utakapowadia, hivyo mafundi /wawakilishi wa waombaji wanaombwa kuhudhuria siku hiyo katika ufunguzi wa zabuni.

12. Maombi ambayo ambayo yatafika baada ya muda tajwa hapo juu hayatapokelewa hata Kwasababu yeyote ile.

  
**MWANAISHAM NASSOR**

**KAIMU MKURUGENZI**

**HALMASHAURI YA MJI TUNDUMA**

